(If A Lot Of People Do Something, Does That Prove That What They Do Is Right?)

Na

Alex S. Silvester

Kama Watu Wengi Wanafanya Jambo, Je Hiyo Inathibitisha Kwamba Wanachofanya Ni Sahihi?

Na

Alex S. Silvester

Nov 1, 2018

Kama Watu Wengi Wanafanya Jambo, Je hiyo Inathibitisha Kuwa Wanachokifanya Ni Sahihi?

Wakati mwingine watu hutazama au hujifunza kuhusu kundi kubwa la watu wanaojihusisha katika mambo ya dini, na kufanya hitimisho hili: “Kama wanachokifanya sio sahihi, kwa nini wengi wanakifanya?” Wengine wanaizungumzia hivi: “Mungu ni lazima awe nao na kuwabariki; vinginevyo kwa nini kuwe na watu wengi katika kundi hili?” tunaweza kusikia pia wengine wakitangaza, “lazima wanafanya kitu sahihi, vinginevyo wasingekuwa na watu wengi hivyo.”

Maneno yote tuliyoona hapo juu tunaweza kuyaweka katika wazo moja au dhana: kama watu wengi, au wingi wa watu wanafanya jambo katika swala la dini, hivyo wanaachofanya ni lazima kiwe sahihi. Kwa maneno mengine, watu wengi wanaojihusissha katika tendo fulani ni ishara kwamba wanachofanya ni kumpendeza Mungu. Je Biblia inaunga mkono jambo hili? Labda mifano ya Biblia inaweza kusaidia katika swala hili.

Safina na Gharika:

Katika siku za Nuhu, “*BWANA akaona ya kuwa maovu ya wanadamu ni makubwa duniani na kwamba kila kusudi analowaza moyoni mwake ni baya tu sikuzote.*” (Mwa. 6:5). Kama matokeo aliamua kuangamiza dunia kwa gharika. “*Lakini Nuhu akapata neema machoni pa BWANA.*” (Mwa. 6:8). Yehova alimwambia mtu huyu sahihi kujenga safina ambamo yeye na familia yake wangeokolewa (Mwa. 6:14-22). Gharika ilipofika, idadi ya “roho nane” pekee waliokolewa katika safina (1 Pet. 3:20). Wengi wa watu walioishi duniani kwa wakati ule walikufa nje ya safina. Kwa shauri hili ilikuwa ni tendo la watu wengi siyo, au si sawa? Katika 1 Pet. 3:20, wale waliokufa nje ya safina wakati wa gharika wanachukuliwa kama “wasiotii.” Tafadhaali angalia: hata kama kundi ndani ya safina lilikuwa ndogo, iliyokuwa na watu wanane, matendo yao yalikuwa sahihi, wakati matendo ya watu wengi (waliokuwa nje ya safina) haikuwa sahihi machoni pa Mungu.

Sodoma:

Mungu alimuhaidi Ibrahimu kwamba kama angepata watu wema katika mji wa Sodoma, hivyo hasinge uangamiza (Mwa. 18:32). Mwishoni, Mungu hakupata wengi walio waaminifu, hivyo mji uliangamizwa. Kabla Mungu hajauangamiza, alituma malaika wake kumuokoa “Lutu mwenye haki”, mke wake, na mabinti zake wawili (2 Pet. 2:7; Mwa. 19:16). Katika tukio hili, ni wazi kwamba ni watu wachache tu waliokolewa katika maangamizi ya mji huu, wakati kundi kubwa waliuawa kwa sababu ya kutokuwa na haki. Swali: katika shauri hili, ni nani aliyempendeza Mungu, watu walioangamizwa ndani ya Sodoma (wengi), au wale waliokimbia mji (wachache)? Jibu liko wazi, siyo?

Wanajeshi wa Israeli Nyikani:

Kati ya wanajeshi 603,550 waliohesabiwa katika mlima Sinai, ni wawili tu, Kalebu na Yoshua walioruhusiwa kuingia nchi ya Kanaani (Hes. 14:28-30). Na vipi kuhusu wengine? Kwa sababu ya kile ambacho Biblia inaita "kutokuamini kwao" hawakurusiwa kuingia katika nchi ya ahadi (Heb. 3:19). Wanajeshi wawili walikuwa waaminifu; wengine hawakuwa. Tunaweza kusema kwamba wengi (wale wanao chukuliwa "wasio amini) kuendana na uthibitisho Mungu? Siyo ngumu. Tena, tunaona kwamba wengi wa watu wanaweza kufanya, hata watu wa dini, wanaona kwamba siyo muhimu kumpendeza Muumba.

Mitume wa Yesu: Labda 100% ya washiriki wa dini hiyo waliungana katika walichofanya. Je hiyo inathibitisha kwamba walichokifanya kilikuwa sahihi kulingana na kweli? Angalia mfano kutoka katika maisha ya mitume wa Yesu. Bwana wetu alipotwaliwa na Yuda Iskariote na watu wengi walioongozana nao mbele ya wakuu wa makuhani ili kujaribiwa na Wayahudi, mitume walifanya nini? Walikimbia! Wangapi waliyokimbia? Aslimia mia moja. "*Mitume wote walimkana, wakaondoka.*" (Mat. 26:56). Mitume wote walimkataa Yesu! Je tunapaswa kuhitimisha kwamba kwa vile wote walifanya hivi, hiyo inathibitisha kwamba Yesu alikuwa kitu sahihi kufanya? Tunafahamu jibu!

Wengi Waliomlilia Yesu Ili Asulubiwe:

Asubuhi ya kusulubiwa kwa Yesu, mkuu wa Kirumi ambaye Yesu alisimama mbele yake, Pilato akawapa Wayahudi chaguo. Alikuwa na wafungwa wawili maalum gerezani, Baraba na Yesu. Angemuachiaa mmoja wao na kumsubisha mwingine. Wakati Pilato alipowauliza kusanyiko lililokuwa mbele yake kwamba, "*Mnataka niwafungulie nani? Baraba au Yesu aitwaye Kristo?*" (Mat. 27:17). Yote yaliyosemwa na kufanywa, Pilato alimwachia huru Baraba, na akamhukumu Kristo hata kufa. Kwa nini? "*Nao wakuu wa makuhani na wazeewakawashawishi makutano ili wamtake Baraba na kumwangamiza Yesu.*" (Mat. 27:20). Angalia tena ni naani aliyelia ili Yesu asulubiwe: walikuwa "wengi". Marafiki, watu wengi walitaka Yesu auawe. Je bado unashawishika kwamba katika shauri lolote, chochote ambacho watu wengi wanafanya au kusema kinapaswa kuwa sahihi? Hakika huwezi kusifu hitaji la wengi la kumuua Mwana wa Mungu asiye na dhambi! Hatuwezi kukosa ukweli huu: wakati watu haowengi waovu walipopiga kelele kwa ajili ya damu ya Yesu, hata kama, "walikuwa na idadi" hawakuwa sahihi.

Ni hitimisho gani tunaweza kupata katika maneno matano ya Biblia ambazo tumeangalia? Ni rahisi. Usidanganyike: idadi ya watu waliokuwa kwenye kundi lile au tendo haithibitishi kama matendo yao ni sahihi au siyo sahihi machoni pa Bwana. tujitahidi kuwa waaminifu kwa Mungu, na tusiwe na shaka kuhusu "tuna" watu wengi au wachache kuliko kundi lingine lilivyo.

Baadhi ya maswali ya mwisho:

Mungu aliwaambia nini wana wa Israeli kuhusu kufuata makundi? "*Usiandaamane na mkutano kutenda uovu…*" (Kut. 23:2).

Je Bwana anaweza kuokoa wengi walioko upande wake? Je Bwana anaweza kuwaokoa wachache wanaoendana naye? Aliwaokoa Waisraeli na jeshi la Gidioni ya watu 300 tu (Waamzi 7). Tutafanya vizuri pia kukumbuka kile ambacho Yonathani, mwana wa mfalme Daudi alisema: "*...kwa maana hakuna la kumzuia BWANA asiokoe kwamba ni kwa wengi au kwamba ni kwa wachache.*" (1 Sam. 14:6).

Yesu alisema nini kuhusu watu wanaongozana kwenda upotevuni na kwenye uzima? "*ingieni kwa kupitia mlango ulio mwembamba; maana mlango ni mpana na njia ni pana iendayo upotevuni, nao ni wengi waingiao kwa mlango huo. Bali mlango ni mwembamba, na njia imesonga iendayo uzimani, nao waionao ni wachache.*" (Mat.7:13-14). Kunaweza kukawa na jibu la wazi katika hitaji letu kuhusu kile watu wengi wanachofanya kama ni sahihi au sio sahihi.

Tumekuwa tukiangalia mara kwa mara tena kuhusu kundi kubwa la watu au wanachokifanya wengi. Lakini vipi kuhusu matendo ya wachache? Kama kundi dogo linapofanya jambo, je ukweli kwamba wanafanya jambo wakiwa wachache inamanisha kwamba matendo yao yanapendeza machoni pa Mungu? Sivyo. Ukweli ni ukweli, na haki ni haki, bila kujali kwamba ni wengi au wachache au wengi wanaotembea katika njia ya Mungu ya haki. Watu wengi, hasaa kundi kubwa katika ulimwengu wa dini, wanadai kuwa wako sahihi kwa sababu ya wengi wanamfuata wahubiri wao.

Kwa ajili ya Kristo, Sadat.